USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

# MIFUMO YETU

**Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI**

**TOLEO NA. 9** **MEI 2019 — JULAI 2019**




# Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini, Suluhisho la Upatikanaji Taarifa Sahihi na kwa Wakati

***Zainab Kitembe Mtaalam wa Ustawi wa Jamii, kutoka OR-TAMISEMI, akitoa uchanganuzi wa takwimu za masuala ya lishe yaliyoingizwa katika Mfumo Jumuishi wa Tathimini na Ufuatiliaji jijini Mwanza (iMES) (Picha; Atley Kuni– TAMISEMI)***

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*“ Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya*

*Ofisi ya Rais-TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani”*

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

# Bodi ya Uhariri


## Mwenyekiti

*Mhandisi. Joseph M. Nyamhanga*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*

## Waandishi

*Atley Kuni - TAMISEMI*
*Mathias Costa - TAMISEMI*
*Jacqueline Sombe – PS3*

## Mhariri Mkuu

*Gladys Mkuchu - PS3*

## Wahariri

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*
*Conrad Mbuya – PS3*

## Msanifu Kurasa

*Gladys Mkuchu – PS3*


## Jarida hili hutolewa na:


*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*
*Blogu: blog.tamisemi.go.tz*
*Facebook: Ofisi ya Rais – TAMISEMI*
*Instagram: ortamisemi*

## Ndani ya Jarida Hili:

**Tahariri……………………………………………………………………………………………...uk 6**

**iMES Tulipotoka, Tulipo na Tunapokwenda…………………………….……………….uk 7**

**Tanzania Yaja na Mfumo Jumuishi wa Tathmini na Ufuatiliaji……………………………..uk 8**

**iMES Mwanga Mpya kwa Watakwimu………………………………………………………...uk 9**

**iMES Mkombozi Masuala ya Lishe……………………………………..…………..…......uk 10**

*TAHARIRI:*

# Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini

Suala la upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati, limekua na changamoto kwa muda mrefu. Hali hii ilisababishwa na kutokuwepo kwa mfumo maalum na nyenzo imara za kukusanya na kuchambua takwimu kutoka vyanzo tofauti.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa ushirikiano na Wizara za Kisekta, Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) na wadau wa maendeleo Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) imesanifu na kutengeneza Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa njia ya kieletroniki ***(intergrated Monitoring and Evaluation Systerm - iMES***) utakaowezesha upatikanaji wa takwimu kutoka vyanzo mbalimbali kutoka sekta zote zilizopo ngazi ya msingi.

Aidha, mfumo huu utakuwa jukwaa muhimu la kupata takwimu zitakazowezesha kufanya shughuli za ufuatiliaji, tathmini, upangaji wa mipango na uandaaji wa bajeti. Vilevile, mfumo utafanikisha uwepo wa taarifa sahihi zinazofanana na kwa wakati ili kuweza kusaidia viongozi na wataalam wa Serikali kufanya maamuzi muhimu kwa ustawi wa nchi yetu.

Mfumo wa iMES kupitia *Muungano Gateway* utapata taarifa kutoka mifumo mingine ya Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma (IFMIS / Epicor), Mfumo wa Mipango, Bajeti na Taarifa (PlanRep), Mfumo wa Usimamizi wa Uhasibu na Utoaji wa Taarifa za Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS), Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS) na Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Vituo vya Kutoa Huduma za Afya (GoTHOMIS).

Sambamba na hiyo, mifumo mingine itakayowasiliana na iMES, ni Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Shule (SIS), Mfumo wa Takwimu za Elimumsingi (BEMIS), Mfumo wa Takwimu za Kilimo (ARDS), Mfumo wa Taarifa za Afya (DHIS2), Mfumo wa Masuala ya Ardhi *(Intergrated Land Management Information Systerm-ILMIS*), Mfumo wa Taarifa ya Usimamizi wa Sekta ya Maji *(Water Sanitation Management Information Systerm-WSMIS),* Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa barabara za Wilaya *(District Roads Management Information System-DROMAS)* na mifumo ya sekta mbalimbali kwa kadri ya mahitaji.

Nichukue fursa hii kutambua mchango mkubwa unaoendelea kutolewa na wadau wa maendeleo PS3 ambao wamekuwa mstari wa mbele katika suala zima la uimarishaji wa mifumo ya sekta za umma kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, kazi hii imefanikiwa kwa kupata ushirikiano mkubwa kutoka Wizara zote za kisekta zilizoshiriki katika hatua mbalimbali za uundwaji wa mfumo huu chini ya uongozi wa Wakala ya Serikali Mtandao (eGA).

Napenda kutoa rai kwa wadau wote kuanzia ngazi za jamii, vituo vya kutolea huduma mpaka ngazi ya Taifa kutumia mfumo huu kupata taarifa sahihi na kwa wakati na kufanya maamuzi kwaajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Nawatakia usomaji mzuri wa Jarida letu la Mifumo Yetu toleo la tisa.

**Mhandisi Joseph M. Nyamhanga**

**Katibu Mkuu, OR-TAMISEMI**

# *iMES Tulipotoka, Tulipo na Tunapokwenda*


Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa njia ya kieletroniki (Integrated Monitoring and Evaluation System-iMES) una lengo la kuwa na upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo chini ya ufadhili wa watu wa Marekani USAID kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma pamoja na Wizara za Kisekata wameweza kufanikisha utengenezwaji wa mfumo huu.

Katika dunia ya leo mahitaji ya takwimu katika Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) ni jambo ambalo haliepukiki.

Mfumo uliotumika awali ujulikanao kama *Local Government Monitoring Database-LGMD* ulikuwa unakusanya takwimu za sekta zote katika ngazi ya Kata kwa kutumia fomu maalum zilizotayarishwa katika mfumo husika na kisha takwimu hizo kuingizwa katika mfumo na Afisa wa ngazi ya Halmashauri. Hata hivyo Mfumo huu ulishindwa kukidhi mahitaji ya muda na wakati wa sasa kwakuwa ulikua ni mfumo wenye kanzi data nyingi zisizokua na mawasiliano (*standalone*) na sio wa kielektroniki.

Hii ilisababisha kudhoofisha mfumo uliokuwepo. Takwimu zilizokusanywa kupitia mfumo wa *LGMD* zilikusanywa pia na mifumo mengine ya Wizara za Kisekta na kufanya kazi mara mbili mbili. Mabadiliko ya matoleo ya mfumo ya mara kwa mara ilisababisha baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia matoleo tofauti tofauti katika kukusanya takwimu za aina moja.

Mtaalam kutoka OR-TAMISEMI ambaye ni Mkuu wa eneo la takwimu Teobard Katabalo, anasema ili mfumo uweze kuhudumia kwa ufanisi na kuwa na tija, Wizara imekasimu madaraka katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na jukumu hilo kupewa mtaalam wa takwimu katika ngazi za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kuwa wasimamizi wakuu wa mfumo huu.



*Wataalamu kutoka OR-TAMISEMI, PS3 na wadau wengine wakiwa kwenye kikao kazi cha kufanyia maboresho ya mfumo wa iMES mkoani Mwanza (Picha; PS3)*

"Mfumo huu wa iMES unakwenda kujibu changamoto ambazo LGMD ilikumbana nazo. Mfumo utakuwa na uwezo wa kuwasiliana na mifumo ya Wizara za Kisekta na kuvuta takwimu tofauti tofauti kulingana na mahitaji ya mtumiaji kupitia Muungano Gateway. Takwimu zote za kisekta zitapatikana kupitia jukwaa moja na hili litarahisisha zoezi la kufanya tathmini na ufuatiliaji na kuzifanya Halmashauri zote kutumia toleo moja la mfumo na maboresho yote wadau watayapata kwa pamoja kwa wakati mmoja," anasema Katabalo

Katabalo anaongeza kuwa mfumo wa iMES utasaidia kuwa na taarifa sahihi ambazo zitasaidia katika tafiti na kufanya maamuzi mbalimbali ya maendeleo kupitia sekta mbalimbali ambazo zitakuwa na taarifa zake. Mageuzi haya ya upatikanaji wa takwimu yatachagizwa na fomu maalum kutoka sekta mbali mbali zitakazo tumika kukusanyia takwimu ambazo hazipatikani katika mifumo ya wizara za kisekta.


Usanifu wa mfumo wa iMES uko tayari na viashiria vya takwimu kwa sekta za Usimamizi wa fedha za umma (*Public Finance Management PFM*), Afya na Wasifu wa Kiuchumi na Kijamii tayari zimeingizwa katika mfumo wa iMES na tayari mfumo umeweza kuzalisha Jedwali la alama za viashiria vya lishe (*Scorecard)* baada ya kuingiza takwimu za viashiria hivyo.

Matarajio na muendelezo wa mfumo kwa sasa ni kupiga hatua za uingizwaji wa viashiria vya sekta mbalimbali ndani ya mfumo ili uweze kubadilishana taarifa na mifumo mingine ya Wizara kwa kuvuta takwimu kutoka katika mifumo ya Wizara husika.

**Mathias Costa na *Atley Kuni - TAMISEMI***

# *Tanzania Yaja na Mfumo Jumuishi wa Tathmini na Ufuatiliaji*

Kuwepo kwa mfumo mmoja wenye uwezo wa kukusanya, kutathimini na kufuatilia taarifa ni moja kati ya hatua kubwa ambazo Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) na Wizara zingine za Kisekta wameweza kupiga kwakuwa itapelekea kuleta ufanisi katika ufanyaji maamuzi pamoja na utawala bora.




***Mchoro unaoonesha namna ambavyo mfumo wa iMES utakavyokuwa unawasiliana na mifumo mingine ya kisekta kupitia Muungano Gateway***

Mfumo wa iMES umeundwa na kusanifiwa na Wataalamu ndani ambao ni wazawa wa Tanzania kwa kujumuisha wataalam kutoka OR-TAMISEMI na PS3. Hivyo kupunguza gharama kubwa zitokanazo na kuwalipa wataalam wa nje. Kuwajengea zaidi wazawa uwezo wa kusanifu na kuunda mifumo mikubwa kama hii pamoja utawezesha mabadiliko na maboresho kufanyika katika muda mfupi zaidi ukilinganisha na kutegemea wataalam wa nje au makampuni binafsi katika maboresho na uundaji wa mfumo huu.

Mfumo wa iMES umetengenezwa kwaajili ya madhumuni ya kuisaidia Serikali katika masuala ya taarifa pamoja na kutatua changamoto ya muda mrefu ya uhifadhi taarifa katika ngazi za utawala.

Milton Ndosi, Mtaalam wa Mifumo kutoka PS3 anasema, "iMES ni mfumo madhubuti unaotazamiwa kutatua changamoto za upatikanaji wa taarifa sahihi kwani umesanifiwa kwa nia ya kumrahisishia mtumiaji wa mfumo kupata taarifa sahihi na kwa wakati. iMES ni mfumo unaowezesha OR-TAMISEMI kukusanya taarifa mbalimbali hata zile ambazo hazikusanywi na mifumo mingine. Mfumo huu unaweza kukusanya taarifa katika ngazi zote za mamlaka za serikali za mitaa yani ngazi ya wizara, mikoa, halmashauri, kata, vijiji na hata ngazi za kutolea huduma. Aidha, mfumo huu una uwezo wa kutoa taarifa jumuishi kwa kujumlisha na kuchakata viashiria katika ngazi ya kutolea huduma hadi ngazi ya wizara kwa ujumla."

Hapo awali, ilikua ni vigumu kwa watumiaji wa mifumo kupata taarifa kutokana na taarifa hizo kuwepo katika mifumo tofauti tofauti isiyowasiliana. Mfumo wa iMES umeunganishwa na Muungano Gateway ambao ni mfumo unaofanya kazi kama uti wa mgongo wa mawasiliano baina ya mifumo katika OR-TAMISEMI. Hiyo iMES itakua ni mfumo unaofanya kazi kama kituo kikuu cha kupata taarifa kwani una uwezo wa kukusanya taarifa zisizokusanywa na mifumo mingine pamoja na kuhifadhi taarifa zipatikanazo kutoka kwenye mifumo mingine baada ya kuvutwa kupitia Muungano gateway.

Ifahamike kuwa mfumo umejikita katika sehemu ya Ufuatiliaji na Tathmini. Hivyo basi itawawezesha watakwimu kufanya kazi kwa ufanisi. Mfumo unawapa uwezo wa kukusanya taarifa kwa wakati tofauti kama kwa siku, wiki mwezi, robo au nusu mwaka hadi mwaka.


Kwa sasa mfumo unakusanya taarifa kuanzia ngazi ya vituo vya kutolea huduma hadi ngazi ya Wizara. Mfumo umeweza kuingiza taarifa za Wizara, Mikoa, Halmashauri, Vituo vya kutolea Huduma za afya na elimu mpaka katika ngazi ya kata. Ambayo kwa ujumla wake umefanikiwa kuingiza viashiria elfu arobaini.

Pamoja na hayo, hadi kufikia sasa iMES imeshaunganishwa na mifumo inayohusisha usimamizi wa fedha za Umma yaani (PFM) mifumo hiyo ni pamoja na PlanRep, EPICOR, FFARS na LGRCIS.

iMES pia itafanya kazi ya kuweka viashiria katika dashibodi yake ili kuweza kutumika katika kufanya tathimini mbalimbali katika Halmashauri mfano tathimini za masuala ya lishe. Suala hilo limeboreshwa kwa kupitia jukwaa la mfumo wa iMES kwani masuala ya tathmini na ufuatiliaji hayakuwa na mfumo mzuri wakuwawezesha kukusanya viashiria.

***Jacqueline Sombe - PS3***

# iMES Mwanga Mpya kwa Watakwimu




***James Mtatifikolo Afisa TEHAMA kutoka OR-TAMISEMI akiwa kwenye ukurasa wa iMES kama unavyoonekana kwenye mfumo (Picha; Atley Kuni-TAMISEMI)***

Kwa muda mrefu, upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi na kwa wakati imekuwa ni jambo lenye kizungumkuti na hata takwimu zinazopatikana zimekuwa zikipishana kutoka chanzo kimoja na kingine, hivyo kupitia Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini (iMES) ni wazi kwamba tatizo hilo litakuwa historia.

Mfumo wa iMES utawezesha kuzalisha taarifa zilizoboreshwa *(Social Economic Profiles, Sector Specific Indicator Performance Reports, M&E Frame Work, Gross Domestic Product (GDP)* masuala ya Pato la Taifa), ripoti mbalimbali za Washirika, kwa muundo tofauti wa mawasilisho katika muundo wa (pdf, grafu na nk) kutumia vigezo mbalimbali vya kuchuja mfano kipindi masuala ya utawala, lakini pia mfumo utawezesha takwimu na taarifa kulingana na miaka husika.

Akielezea juu ya mfumo huu, James Mtatifikolo ambaye ni mtaalam wa TEHAMA, kutoka OR-TAMISEMI, anasema kuwa mfumo wa iMES, sio wa Wizara wala idara moja ya Serikali bali sekta zote.

“Mfumo huu umekuja kutatua tatizo la muda mrefu la upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati, mara kadhaa viongozi kutoka sekta mbalimbali wamekuwa wakitaka kupata taarifa kwaajili ya kufanya maamuzi lakini hatukuwa na jukwaa moja lililowezesha hili, hivyo mfumo utaleta suluhisho la kudumu,” anasema Mtatifikolo.

Mtatifikolo anaongeza kuwa, ufumbuzi huo wa kudumu wa upatikanaji wa takwimu utasadia kuondoa mkanganyiko uliokuwepo hapo awali hususani uwasilishaji wa takwimu kwa wakati kwenye mamlaka zenye uhitaji wa takwimu kwa muda lakini vilevile utaepusha kutofautiana kwa takwimu kutoka chanzo kimoja kwenda chanzo kingine.

“Hii ni ajenda ya kitaifa ndio maana unaona Wizara za kisekta zimeshiriki kikamilifu katika uundwaji wa mfumo, utakumbuka Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa akiweka jiwe la msingi jengo la Taifa la Takwimu mjini Dodoma tarehe 20 Desemba, 2017 alikemea vikali utoaji wa takwimu bila kufuata taratibu na kuonya wale wote watakaofanya hivyo vyombo vinavyo husika visisite kuchukua hatua,” anaeleza Mtatifikolo.

Kauli ya Mhe. Rais pia ilitoa dira na watalaam kuwaza nje ya boksi na kuja na mfumo wa iMES ambao umechochea ubunifu mahiri kupitia wataalam wa ndani. Hii itawezesha kufanya mabadiliko na marekebisho mbalimbali kulingana na mahitaji na maendeleo ya teknolojia. Mfumo utasaidia kupata takwimu sahihi na za uhakika kupitia iMES.

***Atley Kuni -TAMISEMI***

# iMES Mkombozi Masuala ya Lishe



***Baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi OR-TAMISEMI wakishuhudia zoezi la utiliaji saini juu ya masuala ya Lishe baina Wakuu wa Mikoa na Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI, Mhe.Selemani S.Jafo (Mb) kwaniaba ya Makamu wa Rais Mhe. Samiah Suluhu Hassan Jijini Dodoma Desemba, 2017 (Picha; Atley Kuni-TAMISEMI)***

Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini unaozungumza na mifumo mingine ya kisekta na kukusanya takwimu tofauti tofauti *na kutoa taarifa kupitia Muungano Gateway yaani (intergrated Monitoring and Evaluation System -iMES)*, umetajwa kuwa nyenzo mkombozi itakayosaidia kujua hali halisi ya masuala ya lishe kuanzia ngazi ya chini katika kata hadi kufikia mikoani na nchi nzima na kuongeza uwajibikaji ambao ni chachu ya kufanya maamuzi.

Mratibu wa masuala ya Lishe kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mwita Waibe, anasema iMES itasaidia kuongeza uwajibikaji kwenye ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutoa taarifa zilizo sahihi na kwa wakati katika nyanja ya lishe.

"Makamu wa Rais, Samia Hassan Suluhu kupitia Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI, aliingia Mkataba na Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara juu ya masuala ya Lishe katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa lakini katika kipindi chote wakuu wa Mikoa wamekuwa wakiona viashiria vya lishe kwa ngazi za Mikoa tu na sio ngazi za Halmashauri, hivyo wakashauri ipatikane nyenzo itakayowezesha jambo hilo kuwa rahisi. Kwa mantiki hiyo, iMES itakuwa ndio nyenzo itakayotoa mwanga kwa watendaji hao kufahamu hali ya lishe kwenye Halmashauri zao kupitia dashibodi maalum itakayopatikana wakati wote wawapo maeneo yao ya kazi," anaongeza Mwita.

Aidha kuhusiana na taarifa zinazoingizwa katika mfumo wa iMES, kuwa na ubora unaotakiwa, Mtaalam huyo anasema, vipo vyombo vingine vya ufatiliaji ambavyo vitawezesha jambo husika na kazi kubwa ya iMES itakuwa kupokea taarifa ambazo tayari zimechakatwa na kupita katika ngazi zote muhimu za kiutendaji kabla yakuingizwa katika mfumo.

"Lengo letu ni kushusha madaraka kwenye ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo fedha zote zinaelekezwa na utekelezaji kufanyika huko, katika kila hatua taarifa zitachambuliwa na kuchakatwa ipasavyo kabla ya kwenda hatua inayofuata, Taarifa hizi zikishaingizwa na Maafisa Lishe, zitahakikiwa pia na Mganga Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Halmashauri kabla yakumfikia Katibu Tawala wa Mkoa kwaajili ya kuzihakiki na kuzifanya kuwa takwimu muhimu kwa maamuzi" anasisitiza Mwita.

Kuhusiana na mapokeo, Mwita anasema kumekuwepo na mtazamo chanya kutoka kwa viongozi hususani Wakuu wa Mikoa ambao katika tathmini ya kwanza na ya pili walitaka ipatikane nyenzo mahususi ya ufatiliaji na tathmini itakayowasaidia muda wote kuona masuala ya Lishe kwa Halmashauri zao ili waweze kutambua uwajibikaji kwa kila Halmashauri wanayoiongoza na kutoa mwanya wa kutoa maelekezo inapobidi.

Suala la Lishe ni muhimu nchini ambapo hii inaonekana kufuatia Mkutano wa Kitaifa wa Urutubishaji Chakula *(National Summit on Food Fortification)* uliofanyika tarehe 23-24 mwezi Agosti, 2017, ambapo Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Hassan Suluhu alikuwa ni Mgeni Rasmi na aliagiza kuwepo kwa mkataba wa utendaji na Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara kusimamia utekelezaji wa shughuli za Lishe katika Mikoa yao ili kuondoa tatizo la utapiamlo nchini. Katika kufanikisha azma hiyo, OR-TAMISEMI yenye jukumu la kusimamia utekelezaji katika ngazi za Mikoa na Halmashauri, iliandaa mkataba wenye viashiria vya upimaji vipatavyo 11 na Desemba, 2017 Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI, Mhe. Seleman Jafo (Mb), alisainishana mkataba huo kwa niaba ya Makamu wa Rais, na utekelezaji wake kuanza Januari, 2018.

***Na Mwandishi Wetu***